# ELIMU JUU YA PEPO

Mt. Marko 16:9. Naye alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, alimtokea Mariamu Magdalene, ambaye kwamba alimtoa pepo saba.

Wakati Mungu aliponiumba mimi, William Branham, nilikuwapo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Aliumba utu wangu, roho yangu, sikuwa nina ufahamu wa kitu chochote kwa kadiri ya nijuavyo, lakini, nilikuwa pale (Ayubu 38:4 – 7, Mithali 9:22 – 31). Oh, siamini kama mnalipata hili. Lakini sasa, dakika kidogo, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba aliwajua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na Paulo amesema hapa kwamba alituchagua ndani yake kabla ya dunia kuanza (Efeso 1: 3 – 4). Sasa, kulikuwa na sehemu yangu, Orman Neville, na ninyi wote mliopo hapa, mlikuwa ndani ya Yesu Kristo kabla ya dunia kuwepo. Na hapa kuna uchambuzi wangu juu ya hilo: Nafikiri watu wale ambao leo wameshikwa na huyu Roho au roho, ni sehemu ya viumbe wale wa kimalaika, roho zilizozunguka kutoka kwa Mungu, ambazo kamwe hazikuanguka pale mwanzo na zikampinga Shetani Mbinguni ….(Isaya 14: 12 – 15, Ezekieli 28: 11 – 19).

Na theluthi mbili ya dunia iko kwenye dhambi, na zaidi ya hayo, ambapo theluthi mbili ya malaika walitupwa chini (ufunuo. 12:3 – 4), na roho hizi za kishetani, zimekuja na kukaa katika miili ya watu. Unaona kile ninachomaanisha? Ni mapepo ambayo kwanza …..yalikuwepo kwanza na yanakuja ndani ya watu na kuwapa tabia.
Yesu aliwatoa pepo saba kutoka kwa Mariamu Magdalene, 1. Kiburi, 2. Kujisifu, 3. Uchafu, 4. Kunajisi, 5. Ukosefu wa adabu, 6. Wivu, 7. Vita na mambo haya yote, watu wakubwa Unaona? (Luka 8: 1 – 3, Marko 16:9 – 10)

Mapepo haya yako kwenye kiwango cha roho tunaweza kuwaita pia wasiwasi, mkandamizo, majivuno, mapepo ya uchungu yasiyo ya Mungu, ukichaa, roho za dunia, roho za giza, ulevi, uvutaji, mazoea mabaya. Yesu aliziita shetani. Sasa kila mmoja anajua kwamba neno, Shetani linamaanisha mtesaji. Mtu anayetesa ni Shetani, yule mwovu. Magonjwa yote ni shetani. Huwezi ukalielekeza hilo kwa Mungu unaona? Ni la Shetani.

Nabii wa Mungu ameyataja mapepo mengine kwa jinsi ya mwili kama tezi, Kansa au saratani, Nyumonia, baridi yabisi, upofu wa kuotea ngozi mbele, maumivu ya viungo, kifua kikuu, kifafa, athma, magonjwa ya bakteria, vidonda tumboni, uziwi, upofu n.k.

Katika kiwango cha kidini (roho) alitaja roho chafu (Matendo 8:7), roho ya shaka, ushirikina, kutoamini na dhambi. Maranyingi zinakuja kwa namna ya kidini. Umewahi kuona mtu, mapepo ya kiigiza ukristo? Kwa hiyo mapepo yanaweza kufanya kazi miongoni mwa wakristo, na yanaigiza. Ni ya kidini. Yanadanganya. (1Wafalme 22:19 – 29) au yanakuja na fundisho la uongo (wagalatia 6: 6 – 10, 2Kor. 11:1 – 4).

Na inabidi tuyatoe hayo, kuyakemea na kuyalazimisha kumtoka mtu. Kwa sababu katika mamlaka ya Jina la Yesu Kristo, kila pepo lililoko kuzimu linatii (Marko 1:27 – 34, Matendo 3:16, 4:12).

Nabii wa Mungu alisema; Sasa ninamlaani pepo huyu aitwaye kansa katika jina la Yesu Kristo, amtoke mtu huyu.

Lakini sasa, kipi kinaanzisha huu ugonjwa? Sasa, kitu cha kwanza, ni roho kabla haijawa ugonjwa, kama vile tu ulivyokuwa roho kabla hujawa mwanadamu.

Mara nyingine matezi huinamia upande huu, marefu, mapana na kilakitu. Hayana umbo, kwa sababu yanafanana na hiyo roho ambayo haina umbile. Lakini inafanya kukuwa kwa chembechembe, ni mkusanyiko wa chembechembe. Sasa tuseme sasa hivi uwe na tezi au kansa ni chembechembe zinazokua, zinakua, zinakua zinakula, zinanyonya uhai kutoka kwako, zinaishi katika mkondo wa damu. Kuotea ngozi jichoni kunaondoa yale maji maji laini mazito ya jicho na kukua juu yake na kulifunga jicho. Mengine huja na hayawezi …….. Kama kifua kikuu, hiyo kinakuwa kachembe kadogo, sio chochote kabisa ukubwa wake. Na kachembe hako kadogo hufanya tembo, kufanya funza unaona? Sikitu kabisa ikiwa ni chembe.

Na mengine huchukua umbile la mwili, mengine hayachukui. Namengine hayawi chembechembe za uhai. Mengine yanakuwa roho inayoitesa nafsi. utajaribu kuingiza hiyo sehemu ndani. Nitaiacha sehemu hiyo kwa kesho mchana, kama ninaweza, niwapi hiyo nafsi – roho inakotoka, na vipi hapa chini inaingia …………

Kila mtu aliyeketi hapa amejazwa na kitu fulani (Efeso 2:1 – 2) umejazwa na kitu fulani. Huwezi ukaketi pale bila kujazwa na kitufulani. Hayo maisha hukuongoza wewe na hayo maisha yanatawaliwa na roho. Sasa, unaweza ukawa umejazwa na ulimwengu, unapenda dunia au mambo ya dunia (1Yohana2:15 – 17). Mungu akuhurumie wewe. Unaweza ukawa umejaa kanuni kutoka kanisa fulani, maombi fulani kidogo unayosema, unafikiri yataenda ku…..au unaomba mtu fulani aliyekufa, au unafanya aina fulani ya ishara ya msalaba. Mungu akuhurumie wewe.

Na unaweza ukawa umejaa dini, na bado, hilo ni baya. Hiyo ni sahihi. Hiyo ni sahihi. Biblia ilisema siku za mwisho. Watakuwa ni wakidini sana, wakiwa na mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake, jitenge nao (2Tim.3:1 – 5). Kama umejaa dini, wewe ni mtu maskini, dini tu, yote tu kama umejaa kanuni, hujui unachozungumzia juu yake. Kama umejaa dunia, wewe ni kipofu.

Unajua Mungu alifanya nini kwa Sauli? Mungu alimpa roho mbaya amuongoze (1Samweli 16:14 – 15). Kwa hiyo, mtu anapokataa uongozi wa Roho Mtakatifu, au mtu yoyote anapokataa uongozi wa Roho mtakatifu, unaye Shetani ndani yako wa kukuongoza wewe. Hiyo ni sawa kabisa ni Biblia.

Kama mtu anaongozwa na Roho wa Mungu (Rumi 8:14), Mungu atajifunua kwa mtu huyo. Ndiyo, Bwana. Mungu ameahidi hivyo, kwa hiyo, kwa kufanya hivyo tunajua kwamba Roho Mtakatifu anaongoza, na Mungu hulishughulikia hilo.

Tena napenda kusema jambo lingine, yule roho mbaya alianza kumuongoza Sauli, na akamuongoza yeye. Na leo Roho Mtakatifu anapokataliwa ……….. itafanya nini? Utapata roho mbaya akuongoze. Sasa, sikiliza. Sipendi nikuumize wewe, lakini nataka upate hili, unaona. Kama tu ilivyokuwa katika siku zile, iko hivyo hata leo. Hawapendi Roho Mtakatifu awaongoze, hivyo wanapata roho mbaya. Kinafanyika nini na roho hiyo mbaya? Roho mbaya anapenda awaongoze wao sasa.

Na sasa angalia. Hawataki Mungu awe hakimu wao. Na watu leo hawataki Roho Mtakatifu awe mwamuzi wao. Ndio sababu walimkataa Samweli (1Samweli 8:1 – 22), kwa sababu hukumu yake ilikuwa ni ya Mungu, ilikuwa yakimaandiko. Na hawataki kuongozwa na Roho. Na waliukataa na kukubali watu wa kidini na walipata nini? Roho mbaya wa kuwaongoza. Sasa, watu leo hawapendi kuongozwa na Roho Mtakatifu. Hawapendi Roho Mtakatifu awaamue. Sasa hiyo ni kweli, marafiki, hawapendi Roho Mtakatifu awaamue wao.

Kwa hiyo mambo yote unayoyaona yakitendeka duniani, yalianza katika mwanzo, kwa maana mwanzo ni kitabu cha mbegu cha Biblia, mwanzo, kwa hiyo unaona, roho hizo zilikuwa juu ya watu nyuma katika siku hizo, bado zinaishi ndani ya watu leo. Unaona? Shetani anachukua mtu, lakini zile roho zinaendelea kuishi.

Mungu anamchukua mtu wake, lakini roho inaendelea kuishi. Hiyo inamfanya Yesu Kristo yule Jana, leo na hata milele (Waebrania 13:8). Alimchukua Kristo Yesu, lakini Roho, Roho mtakatifu alirudi tena. Na alikuwa ndani ya watu katika Kanisa wakati wote wa nyakati, kwa sababu Mungu anachukua mtu wake, lakini siyo Roho wake. Shetani anachukua mtu wake na unaona roho zile zile, Angalia asili yao.

Kwa mfano; ukiona mtu kama Luka 8:26 – 39, usifikiri kamwe ni yule mtu, ni shetani aliye ndani ya mtu. Sasa, mkichaa yule pale mimbarani usiku ule aliokusudia kuniua pale Oregon…… Lakini ilikuwa ni Shetani aliyekuwa anafanya hivyo.

Huwezi kamwe kumtoa Shetani kwa mtazamo mbaya. Inachukua upendo kufanya hivyo. Na upendo ni nguvu kuu sana iliyoko duniani (1kor. 13:1 – 8). Sasa, kama unaona, Shetani siku zote ni chuki. Chuki ni ya Shetani. Na watu wanapomchukia mtu, kumbuka ni shetani wa kutisha anayepaswa hudharauliwa au kukataliwa. Usifanye hivyo.

Sasa ndani ya yule mtu (kule Oregoni) kulikuwa na roho hizi ambazo ziliachiliwa kuingia kwa nguruwe kule Gadara (Luka 8:26 – 39, Marko 5:1 – 20). Baadhi ya watu maskini hawa walioko kwenye hospitali za vichaa wakigonga vichwa vyao kwenye vyuma vya nondo, za jela kumbuka, Shetani kamwe hafi. Shetani siku zote anaishi, lakini utakuja wakati mashetani lazima yafe. Wataangamizwa kabisa (Ufun. 20:10) Lakini sasa wanaishi, na wanatenda kazi kizazi hadi kizazi, ndani ya watu. Wengine katika sura ya kansa, wengine katika umbile la kifaa, wengine katika namna ya kifua kikuu, wanaingia ndani ya miili, lakini ionekanavyo hawana nguvu mpaka wampate mtu. Wanatenda kupitia mtu, ambayo inatupa wazo lingine, kwamba Roho mtakatifu yupo……….. akiwa dunia yote lakini hawezi kutenda kazi mpaka akupate wewe na mimi.

Sasa, wakati mkutano unaendelea, na roho mbaya yuko kwenye mkutano, huyo roho hana madhara yoyote mpaka ampate mtu ambaye atatenda kazi kwa huyo. Na anapotenda hivyo, kwa hakika anayo madhara, kwa sababu ni roho mbaya. Na Roho mtakatifu yupo hapa, akijaribu kumpata mtu wa kutenda kupitia yeye na anapompata wa kumtumia aweza kufanya yaliyo mazuri.

Unaona, roho hizo mbili, makusudi yao, malengo? Angalia ilivyo. Angalia kazi zao. Angalia matunda yao. (Waefeso 5:9, Rumi 6:21) ndipo unaweza kujua ni roho gani uliyo nayo.

Unasukumwa na roho. Kama huna roho, umekufa. Na kama una roho, inakusukuma maishani mwako. Na kama maisha yako yanazaa matunda ya mkristo (wagalatia 5:22 – 33), hiyo ni Roho ya mkristo.

Sasa, angalia roho hii mbaya. Anapotoka nje, anatembea mahali pakavu akitafuta mahali pa kupumzika. Biblia imesema hakuweza kupaona (Luka 11:24 – 26). Hivyo husema, "Nitarudi mahali nilipotoka". Je umeliona hilo pepo alitoka kwa kupenda kwake na kurudi kwa kupenda kwake? Anarudi tena kwa mtu yule aliyekuwa amempagaa mwanzo, na anakuta nyumba imefagiliwa na kusafishwa, kutakaswa, hukumu yote imeondoka, oh, mwamini mwenyefuraha. Lakini ni tupu na anasema, "Njoni hapa" pepo wengine saba, wabaya kuliko yeye mwenyewe ……… Tafadhali jaribu kulipata hili. Biblia ilisema hiyo ni kweli. Na anarudi tena kwenye nyumba yake.

Mara nyingine tena: Mtu aliye mkiri Kristo awe Mwokozi wake, akaondoa uovu wake, akaacha ulevi wake, akaacha uvutaji wake, uongo wake, wizi wake, huyo ametakaswa, amesafishwa. Nyumba yake imesafishwa, Anajisikia huru. Sasa huyu roho mbaya anarudi tena na anaikuta hiyo nyumba. Hivyo anaenda na kupata pepo saba wengine wabaya kuliko yeye na anakuja kwa huyu mtu, kama mtu mwema wa nyumba hayuko pale kumshikilia asiingie, Imani ya kuamini. Na mtu mzuri wa nyumba yako ni Imani unasema "kaa mbali" (Matayo 12:22 – 29) hiyo hasa. Na Biblia ilisema hali yake ya mwisho ya mtu huyo ni mbaya mara saba zaidi kuliko mwanzoni. Sasa kama hii nyumba ingekuwa imekaliwa, aliporudi asingeweza tena kuingia.

Shetani hatulii, nguvu za mapepo zinazunguka. Uponyaji, wokovu, utakaso, unadumu kadiri ya imani inavyodumu. Unapoteza imani kwa kukiri udhaifu.

Sasa, marafiki, siwaambii haya kutokana na saikolojia ya aina fulani. Nimeshughulika (kutoa) na mapepo kwa miaka mingi na mnajua hilo. Kama tu mngejua jambo lenyewe, baada ya ibada imeisha wakati wa usiku, kile kinachoendelea wakati mwingine. Hamjui. Kumbuka, unapoenda kinyume na roho, ni vizuri ujue kile unachozungumza. Usisimame pale na kuendelea tu kimzaha, kwa sababu haitakufanyia jambo zuri. Lakini inapobidi hasa pepo akutii, inabidi alitambue hilo. Siyo vile unavyopiga kelele kwa nguvu; siyo mafuta mengi unayoweka. Ni kile kilichoko nyuma hapa (moyoni) hicho atakitambua. Ni kweli (Marko 6:12 – 13).

Leo ni jambo la kutisha. Watu wametawanyika huko na huko. Nilisimama wiki chache zilizopita mahali ambapo kuna hema kubwa iliyosimamishwa, ambapo mtu alisema anaweza akatoa pepo wabaya, ambalo sina shaka nalo hilo. Lakini pepo wabaya hawatolewi kwa ukatili wa kuishi maisha yasiyo. Silaha kubwa yenye nguvu iliyoko duniani ni upendo.

Ndani yako ni kitu kimoja, mahali pamoja, Na mahali hapo ni sawa Mungu alivyopaweka kwa kila mtu kutoka Adamu na Hawa; utashi wa kuamua. Unapenda uishi au unapenda ufe, moja wapo upendalo. Umewekwa kimsingi katika uhuru wa kuamua, na roho yoyote utakayoiacha ikutawale italeta (itazaa) matunda. Maisha yako yatatawaliwa na kile kilichoko ndani. Watu wengi hutegemea hisi hizi tano zilizoko nje. Ni nzuri, hakuna kitu kinyume nazo, kama zinakubaliana na hisi hii ya sita (imani), Na roho hizi zinaweza kuwa aina mbili tu, moja ni Roho ya Mungu, na nyingine ni roho ya Shetani. Huwezi kuwatumikia mabwana wawili kwa mara moja (Matayo 6:24) umejitolea kikamilifu kwa mmoja au kujitolea kwa mwingine. Na kama unaroho wa Mungu ndani yako (Warumi 8:9) unayo imani, na utaamini kila Neno la Mungu lililoandikwa.

**Nukuu za kiingereza:**

Maswali na majibu juu ya kitabu cha Mwanzo", Aya 21, Ishara za kiroho za wakati", Aya 67/, kung'ang'ania (62 – 0608), Aya 115/, Simama tu na uone" Aya 52/, mahali alipochagua Mungu pakuabudia (65 – 0220), Aya 127/, Tumaini letu liko ndani ya Mungu Aya 48/, Elimu ya pepo 1, Kiwango cha mwili Aya 42/47, Kwa nini tumepewa Roho Mtakatifu, Aya 137/ Mfalme aliyekataliwa (60 – 0610), Aya 90 – 94/, Ndipo Yesu akaja akaita (64 – 0417) Aya 10 – 11 maswali na majibu (59 – 1223) Aya 36 – 40/, Umoja wa kuungana, Uk 8/, kuwekeza (63 – 0803) Aya 59 magonjwa na mateso Aya 26 – 28/, Kwa nini watu wanayumba huku na huku Uk. 28/, kung'ang'ania (62 – 0218) Aya 23.

---

Jiwe la kiroho la kujengea no. 142 kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii,
iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69, – D – 75328 Schomberg, Germany
simu (+49) 7235 -7613, Fax (+49) 7235 – 3306.

---

Atakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia. Na kazi ya haraka itaizunguka dunia zile mbegu zitaingizwa katika magazeti na vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyochaguliwa kimbele imesikia hilo (Ndg. Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho Uk. 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E.Y. Kanju*
*Box 5138, Tanga*
*E-mail: chaelika@Hotmail.com*
*cellphone: 0784 704299*